JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MKAKATI WA USAWA WA KIJINSIA KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU 2025/2026 – 2029/2030

OKTOBA, 2025

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# MKAKATI WA USAWA WA KIJINSIA KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU 2025/2026 – 2029/2030

**Oktoba, 2025**

# YALIYOMO

**ORODHA YA VIFUPISHO** ........ iv

**UFAFANUZI WA ISTILAHI** ........ v

**DIBAJI** ........ ix

**SURA YA KWANZA** ........ 1

**UTANGULIZI** ........ 1

1.1 Maelezo ya Awali ........ 1

1.2 Hali Halisi ........ 1

1.3 Wigo wa Mkakati ........ 2

1.4 Maandalizi ya Mkakati ........ 3

**SURA YA PILI** ........ 4

**CHIMBUKO LA KISERA NA KISHERIA** ........ 4

2.1 Msingi wa Kisera ........ 4

2.2 Chimbuko la Kisheria ........ 4

2.3 Nyaraka Nyingine ........ 5

**SURA YA TATU** ........ 6

**DIRA, DHIMA, LENGO KUU NA MALENGO MAHUSUSI** ........ 6

3.1 Dira ........ 6

3.2 Dhima ........ 6

3.3 LengoKuu ........ 6

3.4 MalengoMahususi ........ 6

**SURA YA NNE** ........ 8

**MIKAKATI YA UTEKELEZAJI** ........ 8

4.1 Kuongeza Uelewa wa Dhana za Jinsia ........ 8

4.2 Kuandaa na Kuboresha Sera, Kanuni, Programu, Miongozo pamoja na Kutenga Rasilimali za Utekelezaji ........ 8

4.3 Kuongeza Udahili na Ubakishwaji wa Wanafunzi Unaozingatia Haki, Uwiano na Usawa wa Kijinsia ........ 8

4.4 Kuzingatia Haki na Usawa wa Kijinsia katika Ajira, Kujiendeleza Kitaaluma, Kitaalamu pamoja na Majukumu ya Ufundishaji, Utafiti na Ushauri Elekezi 9

4.5 Kuimarisha Haki, Usawa na uwiano wa Kijinsia katika Uongozi na Ushiriki katika Ngazi za Maamuzi ........................................................................ 10

4.6 Kuimarisha Haki, Usawa na Uwiano wa Kijinsia katika Michezo na Burudani, Upatikanaji wa Elimu na Huduma za Afya ya Uzazi, Afya ya Akili, Magonjwa Yanayoambukiza na Yasiyoambukiza........................................................11

4.7 Kuzingatia Usawa wa Kijinsia katika Maadili na Malezi yanayozingatia Mila na Desturi Chanya za Kitanzania..................................................................11

4.8 Kuandaa na Kuboresha Mitaala na Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia kwa Kuzingatia Haki na Usawa wa Kijinsia ...................................................... 12

4.9 Kuanzisha na Kuimarisha Huduma za Ushauri na Unasihi Zinazozingatia Haki, Usawa na Uwiano wa Kijinsia.............................................................. 13

4.10 Kuimarisha Ulinzi na Usalama kwa Kupinga na Kutokomeza Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia kwa Kuzingatia Haki na Usawa .......................... 13

**SURA YA TANO........................................................................................ 15**

**UFUATILIAJI NA TATHMINI ..................................................................... 15**

5.1 Utangulizi ......................................................................................... 15

5.2 Ufuatiliaji.......................................................................................... 15

5.3 Tathmini ........................................................................................... 16

5.4 Muundo na Majukumu ya Kitaasisi.........................................................16

5.5 Utoaji wa Taarifa ................................................................................17

5.6 Hitimisho .......................................................................................... 18

**KIAMBATISHO 1: MPANGO WA UTEKELEZAJI .......................................... 19**

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ACRWC** | The African Charter on the Rights and Welfare of the Child (Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto) |
| **AZAKI** | Asasi za Kiraia |
| **CEDAW** | Convention on the Elimination of All Forms of Discrimination Against Women (Mkataba wa kuondoa aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake) |
| **CRC** | Convention on the Rights of the Child (Mkataba wa Haki ya Mtoto) |
| **MTAKUWWA** | Mpango kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto |
| **SDGs** | Sustainable Development Goals (Malengo ya Maendeleo Endelevu) |
| **STUH** | Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati |
| **TAKUKURU** | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| **TAMWA** | Tanzania Media Women Association (Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania) |
| **TCU** | Tanzania Commission for Universities (Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania) |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **WMJJWM** | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu |
| **WyEST** | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |

# UFAFANUZI WA ISTILAHI

Kwa madhumuni ya mkakati huu, maneno yafuatayo yanatafsiriwa kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| **Afua** | Shughuli zinazotekelezwa na taasisi kwa ajili ya kutatua changamoto zilizopo. |
| **Elimu Jumuishi** | Elimu inayoyaweka pamoja makundi yote ya wajifunzaji kwa kuzingatia haki na usawa kulingana na mahitaji ya kila kundi. |
| **Elimu Maalumu** | Elimu inayotolewa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji ambao kwa sababu mbalimbali, wanahitaji msaada wa ziada na mbinu za ufundishaji zinazoendana na mahitaji yao. Dhumuni la elimu hiyo ni kushiriki na kufikia malengo ya kujifunza katika mpango wa elimu. |
| **Haki Sawa Kijinsia** | Hali ya watu wote kuwa na haki sawa katika mgawanyo wa majukumu pamoja na fursa sawa katika kunufaika na rasilimali, kupata maendeleo, elimu, huduma za jamii pamoja na kushiriki kwenye maamuzi. |
| **Jinsi** | Hali ya kimaumbile inayomtofautisha mwanamume na mwanamke ambayo mtu huzaliwa nayo. Tofauti za kijinsi ni za kibaiolojia na hazibadiliki. |
| **Jinsia** | Mahusiano yanayojengwa na jamii, mila, tamaduni na desturi kuhusiana na mgawanyo wa majukumu, hadhi, upatikanaji na umiliki wa raslimali kati ya wanawake na wanaume. |
| **Jitihada za Makusudi** | Hatua zinazotoa kipaumbele kwa wanawake ili kuwawezesha kurekebisha kutokuwepo kwa usawa katika kupata rasilimali, mamlaka au fursa mbalimbali. Aidha, jitihada ni uwezo wa dhamira ya dhati kwa muda fulani uliowekwa ili kufidia hasara na mapengo ya kihistoria na kijamii yanayozuia ushiriki wa wanawake katika fursa mbalimbali. |
| **Mahitaji Maalumu** | Haya ni mahitaji mahususi au ya ziada yenye lengo la kuwasaidia na kuwawezesha watu wenye changamoto za kimwili, kitabia, kijamii na kiakili. |

| | |
|---|---|
| **Mahitaji ya Kijinsia** | Mahitaji muhimu ya mwanamke au mwanaume kulingana na majukumu ya kijinsia yaliyoelekezwa kwake na jamii husika. Mahitaji ya Kijinsia yako ya aina mbili ambayo ni mahitaji ya kawaida ya kijinsia (Practical gender needs) na Mahitaji ya kimkakati ya kijinsia (Strategic gender needs). |
| **Majukumu ya Kijinsia** | Majukumu tofauti kati ya wanawake na wanaume yaliyobainishwa na kuendelezwa kijamii, kwa mfano, kupika, kufua, kuteka maji na kusafisha nyumba yanavyotambulika kama majukumu ya kijinsia ya wanawake badala ya kuwa ni majukumu ya wote. |
| **Makundi Maalumu** | Makundi haya yanajumuisha wazee, wanawake, watoto, wajane, wagumba, wafanyabiashara ndogo ndogo na watu wenye ulemavu. |
| **Matukio ya Dharura** | Haya ni mambo yanayojumuisha majanga mbalimbali kama vile moto, mafuriko, magonjwa, vifo, njaa, ukame na mambo mengine yanayoweza kujitokeza. |
| **Mfumo Dume** | Huu ni mfumo unaompendelea mwanamume na kumkandamiza, kumnyonya na kumdhulumu mwanamke haki yake katika nyanja mbalimbali ikiwemo elimu, uongozi na umiliki wa mali. |
| **Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii** | Ni huduma endelevu katika kutatua matatizo ya kijamii, kihisia na kisaikolojia ili kulinda ustawi wa mtu mmoja mmoja, familia na jamii. |
| **Msongo wa Mawazo** | Hali ya mfadhaiko wa akili anaoupata mtu kutokana na shida, taabu, dhiki, matatizo au changamoto zinazomkabili katika maisha ya kila siku. |
| **Rushwa ya Ngono** | Kitendo cha mtu mwenye nafasi ya madaraka au mamlaka kutumia vibaya nafasi yake kwa kulazimisha, kushawishi, au kuomba ngono ili kubadilishana/kutoa/kupewa huduma/haki anayostahili au asiyostahili. |
| **Taasisi za Elimu ya Juu** | Vyuo vinavyotoa elimu ya Stashahada ya Juu, Shahada, Shahada ya Uzamili/Umahiri na Shahada ya Uzamivu zilizothibitishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi au Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. |

| | |
|---|---|
| **Uanishaji wa Takwimu za Jinsia** | Uchambuzi na uandaaji wa takwimu unaozingatia jinsia katika shughuli za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisheria, kiteknolojiana maeneo mengine. |
| **Ubaguzi wa Kijinsia** | Hali ya kutojali, kumnyanyapaa mtu au kumbagua kutokana na jinsi yake, yaani kuwa mwanamke au mwanaume. |
| **Ujumuishwaji wa Kijinsia** | Mchakato unaojumuisha masuala ya kijinsia katika sera, kanuni, mipango, programu na shughuli zote za jamii na taasisi kwa lengo la kufikia usawa wa kijinsia. |
| **Ukatili wa Kijinsia** | Kitendo chochote chenye madhara anachofanyiwa mwanamke/ mwanamumе na kumuathiri kimwili, kiafya, kiuchumi, kiakili au kisaikolojia. |
| **Ukondoeshaji** | Uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera, sheria, kanuni, mipango, bajeti na programu kwa ajili ya kufikia usawa wa kijinsia. |
| **Unasihi** | Mchakato wa kumsaidia na kumwongoza mtu mwenye changamoto ili kupata utatuzi au kukubaliana na hali inayomkabili. |
| **Unyanyasaji wa Kingono** | Kitendo chochote kinachoumiza cha udhalilishaji wa kingono anaofanyiwa mtu wa jinsi nyingine kwa makusudi na kwa namna isiyofaa au isiyokubalika kwa njia ya matamshi, ishara, picha, ujumbe au kimwili. |
| **Unyonyaji na Unyanyasaji wa Kingono** | Kitendo chochote kinachoumiza mtu kinachofanywa na mtu mwingine mwenye nafasi ya madaraka au mamlaka anapotumia vibaya nafasi yake kumdhulumu na kumdhalilisha kingono mtu wa jinsia nyingine aliye kwenye nafasi ya chini au mnyonge. |
| **Usawa wa Kijinsia** | Haki sawa kati ya wanawake na wanaume, wasichana na wavulana, watoto wa kike na wa kiume. |
| **Uwiano wa Kijinsia** | Dhana ya haki na usawa katika mgawanyo wa rasilimali, faida na wajibu kati ya wanaume na wanawake, wasichana na wavulana katika nyanja zote za maisha. Katika kuhakikisha uwiano sawa, ni muhimu kuweka hatua chanya za muda mfupi au mrefu ili kufidia upungufu wa kihistoria na kijamii unaozuia wanawake kupata fursa sawa na wanaume. |

| | |
|---|---|
| **Wadau** | Dhana inayojumuisha Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Taasisi za Elimu ya Juu za Umma na Binafsi, Taasisi za Dini na AZAKI zinazohusika katika Mkakati huu. |
| **Wafanyakazi** | Watumishi wa taasisi husika ambao ni wanataaluma na watendaji. |
| **Watoa Huduma** | Dhana inayojumuisha kampuni na watu binafsi wanaoendesha shughuli mbalimbali ndani ya taasisi kama vile: - malazi, usafi, ulinzi, usafiri, chakula, machapisho ambao siyo wafanyakazi wa taasisi husika. |

# DIBAJI

Mkakati wa Usawa wa Kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu wa Mwaka 2025/26-2029/30 ni moja ya juhudi za Serikali katika kuimarisha usawa wa kijinsia katikaTaasisi za Elimu ya Juu. Mkakati huu umeandaliwa ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 toleo la mwaka 2023, Sera ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake 2023 pamoja na Sera ya Elimu Zanzibar ya mwaka 2006. Lengo kuu la Mkakati huu ni kuimarisha mifumo na miundombinu itakayowezesha ufikiaji wa usawa wa kijinsia na Elimu Jumuishi katika Taasisi za Elimu ya Juu. Mkakati umekusudia kukuza na kuimarisha ustawi wa Elimu ya Juu, kuepuka ukandamizaji, unyanyasaji na ukatili wa kijinsia kwa wafanyakazi, wanafunzi, watoa huduma na wanajamii katika taasisi za elimu za juu ili kuweka mazingira salama na rafiki yatakayowezesha utekelezaji wa majukumu yao.

Aidha, kuandaliwa kwa Mkakati huu ni mwendelezo wa utekelezaji wa mikataba ya kimataifa na kikanda inayohusu uimarishwaji wa usawa wa kijinsia na ujumuishwaji kama vile, tamko namba 1.2 la Haki za Binadamu (1948); Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (1979) na Azimio la Ulingo wa Beijing (1995).

Kwa msingi huo, Serikali imedhamiria kutekeleza Mkakati huu kutokana na kutambua thamani na umuhimu wa kuweka mazingira salama na wezeshi katika Taasisi za Elimu ya Juu kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Serikali kupitia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023 imetamka wazi kuwa itaendelea kushirikiana na wadau, kuhakikisha masuala ya ukatili wa kijinsia, yanajumuishwa katika mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

Mkakati unaelekeza afua na mbinu zitakazotumika katika kuimarisha usawa wa kijinsia na kuweka mazingira bora na salama ya kufundishia, kujifunzia na kufanya kazi. Mkakati huu unahamasisha na kuratibu juhudi za pamoja za wadau na kuimarisha uhusiano baina ya wafanyakazi, wanafunzi, watoa huduma na wanajamii wote katika kuongeza kasi ya uwekaji na uimarishwaji wa haki na usawa wa kijinsia. Aidha, `Mkakati unatoa mwelekeo wa jumla na mahususi katika utekelezaji wa afua za kuimarisha haki na usawa kwenye Taasisi za Elimu ya Juu, ikiwa ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa rasilimali zitakazosaidia utekelezaji wa afua za uimarishaji wa usawa wa kijinsia.

Wizara inatarajia Mkakati huu utatumika kama nyenzo ya kuwezesha ukondoeshaji wa usawa wa kijinsia katika Sera, Kanuni, Mipango, Miongozo, Programu na Bajeti za Taasisi za Elimu ya Juu ili kukuza haki na usawa wa kijinsia. Vilevile, utaongeza kasi ya mabadiliko katika kutokomeza ubaguzi na ukatili wa kijinsia na kuzingatia Elimu

Jumuishi. Uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika uendeshaji wa shughuli zote za Taasisi za Elimu ya Juu, utajenga utamaduni wa kutambua uwezo na mchango wa kila mmoja hivyo kuongeza thamani ya Elimu ya Juu kwa jamii.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatoa shukurani za dhati kwa Wizara za kisekta, idara na taasisi zilizowezesha Mkakati huu kukamilika. Shukrani hizo ziende kwa Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali-Zanzibar, Taasisi za Elimu ya Juu za Umma na Binafsi, Jeshi la Polisi Tanzania, na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).



Prof. Carolyne I. Nombo

**KATIBU MKUU**

# SURA YA 1 UTANGULIZI

## 1.1 Maelezo ya Awali

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inathamini na kutekeleza afua za kujenga na kuimarisha usawa wa kijinsia na haki za binadamu katika maeneo yote ya kijamii zikiwemo taasisi za elimu ya juu.Aidha, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na marejeo yake, Ibara ya 12, 13, 22 na 23 zinasisitiza usawa na heshima kwa binadamu kama lengo la kuwa na jamii yenye usawa, haki na uhuru kwa wote. Hatua hii inalenga kuwezesha ushiriki wa kila mmoja kutumia kikamilifu uwezo, vipaji na vipawa alivyonavyo katika kutekeleza majukumu yake kama vile uzalishaji mali, kushiriki katika nafasi za uongozi na maamuzi.

Serikali imedhamiria kutekeleza na kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo mwaka 2030. Kwa muktadha wa Mkakati huu, serikali imezingatia lengo namba 3, 4 na 5 ili kuweka mazingira ya haki na usawa katika Taasisi za Elimu ya Juu. Lengo namba 3 linahamasisha afya bora kwa watu wote wakiwemo wanajumuia wa Taasisi za Elimu ya Juu ili kukabiliana na changamoto za magonjwa ya afya ya akili, magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Lengo namba 4 linasisitiza kujenga mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia katika Taasisi za Elimu ya Juu bila ubaguzi wowote. Kadhalika, lengo namba 5 linakusudia kutokomeza ukatili na ubaguzi dhidi ya wanawake na wanaume ili kutoa fursa sawa katika upatikanaji wa elimu.

## 1.2 Hali Halisi

Uzoefu unaonesha kuwa uzingatiaji wa haki, usawa wa kijinsia na elimu jumuishi katika Taasisi za Elimu ya Juu bado una changamoto. Pamoja na kukosekana kwa uelewa wa pamoja wa dhana husika, utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika taasisi hizo umekosa jicho la haki, usawa wa kijinsia na elimu jumuishi. Mathalani, tofauti za usawa wa kijinsia zimekuwa zikidhihirika katika nyanja mbalimbali za uongozi, taaluma, ajira na udahili. Takwimu za Tume ya Vyuo Vikuu (TCU, 2022) zinaonesha kuwa udahili katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2021/2022 ulikuwa ni 295,037 kwa wanafunzi wakiume na 229,931 kwa wanafunzi wa kike. Takwimu za mwaka 2018 zinaonesha kuwa wanafunzi wa kike waliojiunga na elimu ya juu ni 40.3% ikilinganishwa na wakiume ambao ni 59.7%.Wanafunzi wa kike waliojiunga na masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati ni 33.6% tu.

Hali kadhalika, utafiti uliofanywa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (2020) katika Taasisi za Elimu ya Juu ulibainisha uwepo wa vitendo vinavyoathiri usawa wa

kijinsia na kuendeleza rushwa ya ngono. Vitendo hivyo hufanywa na wanafunzi pamoja na watumishi ambapo 63% ya wanafunzi na 76.5% ya watumishi waliohojiwa, walikiri uwepo wa rushwa ya ngono sababu kubwa ikiwa ni ukosefu wa maadili. Sababu nyingine zilizotajwa ni pamoja na ushawishi wa mtu mwenye mamlaka, mfumo wa utoaji wa taarifa kutokuwa rafiki na mfumo dhaifu wa kushughulikia rushwa ya ngono. Aidha, utafiti uliofanywa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) 2019 ulionesha kuwepo kwa viashiria vya ukatili wa kijinsia na rushwa ya ngono katika Taasisi za Elimu ya Juu. Hivyo, tatizo hili katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini linahitaji kuangaliwa kwa ukaribu kutokana na madhara yanayojitokeza kama vile:

i. Kuongezeka kwa changamoto ya afya ya akili;

ii. Ugonjwa wa sonona/hofu iliyopindukia na kutojiamini;

iii. Kupata magonjwa ya UKIMWI na magonjwa ya ngono;

iv. Vifo vitokanavyo na unyanyasaji/ukatili;

v. Ulemavu wa kudumu;

vi. Mimba zisizotarajiwa;

vii. Kuongezeka kwa umaskini wa kipato;

viii. Baadhi ya wasichana na wavulana kushindwa kuendelea na masomo; na

ix. Kuongezeka kwa wahitimu wasio mahiri katika fani mbalimbali.

Hivyo, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeandaa Mkakati wa Usawa wa Kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu kama nyenzo itakayosaidia kukabiliana na changamoto zote za kijinsia zinazojitokeza. Mkakati huu unatoa mbinu na namna bora ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali ili kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030 malengo yaliyokusudiwa yanakuwa yametekelezwa.

Ili kuweka mazingira bora, salama na wezeshi ya ufundishaji na ujifunzaji, Mkakati wa Usawa wa Kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu utatumika sanjari na sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali.

## 1.3 Wigo wa Mkakati

Mkakati huu utatumika katika Taasisi za Elimu ya Juu, za umma na binafsi za Tanzania Bara na Zanzibar. Mkakati huu, utatumiwa na wafanyakazi, wanafunzi, watoa huduma na jamii yote iliyomo ndani ya taasisi husika ili kuwa na uelewa wa pamoja wa masuala ya haki na usawa wa kijinsia na elimu jumuishi.

## 1.4 Maandalizi ya Mkakati

Mkakati wa Usawa wa Kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini umeandaliwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali katika ngazi tofauti ukihusisha wizara mbalimbali za kisekta pamoja na Taasisi za Elimu ya Juu wakiwemo wafanyakazi na wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu na watoa huduma pamoja na asasi za kiraia.

# SURA YA 2 CHIMBUKO LA KISERA NA KISHERIA

## 2.1 Msingi wa Kisera

Mkakati huu umetokana na sera mbalimbali zinazosimamia masuala ya haki na usawa wa kijinsia, elimu na elimu jumuishi nchini kama vile:

i. Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023;

ii. Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023;

iii. Sera ya Elimu ya Zanzibar ya Mwaka 2006;

iv. Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008; na

v. Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2008.

## 2.2 Chimbuko la Kisheria

Mkakati huu umetokana na sheria mbalimbali zinazosimamia haki na usawa wa kijinsia na elimu jumuishi kama vile:

i. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara, sehemu ya tatu, ibara ya 12 na 13;

ii. Katiba ya Zanzibar ya 1984, Toleo la 2010;

iii. Sheria ya Ushahidi, Sura ya 16;

iv. Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366;

v. Kanuni za Utumishi wa Umma, mwaka 2022;

vi. Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma ya toleo la 2023;

vii. Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329;

viii. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20;

ix. Sheria ya Mtoto, Sura ya 13;

x. Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298;

xi. Sheria ya Vyuo Vikuu 2005; na

xii. Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16.

## 2.3 Nyaraka Nyingine

Nyaraka nyingine zilizohusika katika uandaaji wa Mkakati huu ni pamoja na:

i. Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake-CEDAW (1979);

ii. Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (1989);

iii. Malengo ya Maendeleo Endelevu - SDGs (2030);

iv. Mkataba wa Haki za Mtoto - CRC (1989);

v. Ajenda ya Maendeleo ya Afrika Tuitakayo (2063);

vi. Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto - ACRWC (1990);

vii. Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi 2022-2026;

viii. Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi 2021/2022 - 2025/2026;

ix. Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Dawati la Kutokomeza Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia katika Maeneo ya Umma wa Mwaka 2023;

x. Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050;

xi. Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia 2005;

xii. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050;

xiii. Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano III (2021/22 – 2025/26);

xiv. Mwongozo wa Uanzishaji, Uendeshaji na Ufuatiliaji wa Dawati la Jinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati (2021);

xv. Mwongozo na Taratibu za Utoaji wa Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii (2020); na

xvi. Azimio la Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu 1948.

## SURA YA 3 DIRA, DHIMA, LENGO KUU NA MALENGO MAHUSUSI

### 3.1 Dira

Kuwa na Taasisi za Elimu ya Juu zenye mfumo unaozingatia haki, usawa wa kijinsia, elimu jumuishi na zinazopinga ukatili na unyanyasaji wa kijinsia.

### 3.2 Dhima

Kukuza haki na usawa wa kijinsia, kuongeza kasi ya mabadiliko katika kutokomeza ubaguzi, ukatili na unyanyasaji wa kijinsia na kuzingatia elimu jumuishi kwenye Taasisi za Elimu ya Juu.

### 3.3 Lengo Kuu

Kuimarisha haki na usawa wa Kijinsia Katika Taasisi za Elimu ya Juu ili kuwa na Mazingira bora na jumuishi ya kujifunzia na kufanyia kazi.

### 3.4 Malengo Mahususi

Katika kufanikisha lengo kuu, Taasisi za Elimu ya Juu zinapaswa kutekeleza malengo mahususi yafuatayo:

i. Kuongeza uelewa wa dhana za jinsia;

ii. Kuandaa na kuboresha sera, kanuni, programu, miongozo pamoja na kutenga rasilimali za utekelezaji;

iii. Kuongeza udahili na ubakishwaji wa wanafunzi unaozingatia haki, uwiano na usawa wa kijinsia;

iv. Kuzingatia haki na usawa wa kijinsia katika ajira, kujiendeleza kitaaluma, kitaalamu pamoja na majukumu ya ufundishaji, utafiti na ushauri elekezi;

v. Kuimarisha haki na usawa wa kijinsia katika uongozi na ushiriki katika ngazi za maamuzi;

vi. Kuimarisha haki, usawa na uwiano wa kijinsia katika michezo, burudani, upatikanaji wa elimu, huduma za afya ya uzazi, afya ya akili na magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza;

vii. Kuzingatia usawa wa kijinsia katika maadili na malezi yanayozingatia mila na desturi chanya za kitanzania;

viii. Kuandaa na kuboresha mitaala na mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia haki na usawa wa kijinsia;

ix. Kuimarisha na kuanzisha huduma za ushauri na unasihi zinazozingatia haki, usawa wa kijinsia na ujumuishi; na

x. Kuimarisha ulinzi na usalama kwa kupinga na kutokomeza ukatili na unyanyasaji wa kijinsia kwa kuzingatia haki na usawa.

# SURA YA 4 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

## 4.1 Kuongeza Uelewa wa Dhana za Jinsia

Kuna umuhimu wa kuongeza uelewa kuhusu dhana ya jinsia miongoni mwa wanafunzi, wafanyakazi na watoa huduma katika Taasisi za Elimu ya Juu. Ili kuongeza na kuboresha uelewa wa dhana za ujinsia, kwa kuzingatia mila na desturi chanya za kitanzania, Taasisi za Elimu ya Juu kwa kushirikiana na wadau zinapaswa kuandaa na kutekeleza mikakati ifuatayo:

i. Kutoa elimu ya dhana za jinsia kwa kuzingatia mila na desturi chanya za kitanzania;

ii. Kuingiza masuala ya kijinsia katika shughuli zote za taasisi; na

iii. Kuwajengea uwezo wanajumuiya wataasisi kuhusu utoaji huduma stahiki kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia.

## 4.2 Kuandaa na Kuboresha Sera, Kanuni, Programu, Miongozo pamoja na Kutenga Rasilimali za Utekelezaji

Uzoefu unaonesha kuwa sera, kanuni, programu na miongozo iliyoandaliwa na taasisi imepitwa na wakati au haipo. Pia, kuna baadhi ya Taasisi za Elimu ya Juu hazina sera zinazoongoza na kuratibu masuala ya kijinsia na hazina mikakati ya utekelezaji inayokidhi na kuakisi mahitaji ya taasisi husika. Vilevile, kuna changamoto ya utengwaji wa rasilimali za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wake. Taasisi, kwa kushirikiana na wadau, zinapaswa kuandaa na kutekeleza mikakati ifuatayo:

i. Kuandaa na kuboresha sera, kanuni, programu na miongozo inayozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia;

ii. Kujenga uelewa kwa wanajumuiya kuhusu uwepo, umuhimu na matumizi ya nyaraka hizo; na

iii. Kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa kuandaa na kuboresha nyaraka hizo.

## 4.3 Kuongeza Udahili na Ubakishwaji wa Wanafunzi Unaozingatia Haki, Uwiano na Usawa wa Kijinsia

Uzoefu unaonesha kuwa zipo changamoto za jumla za kufikia usawa wa kijinsia katika udahili wa wanafunzi kwenye Taasisi za Elimu ya Juu. Vilevile, upo udahili pungufu

kwa wanafunzi wa kike ikilinganishwa na wale wa kiume kwenye fani za Sayansi, Teknololjia, Uhandisi na Hisabati (STUH). Imebainika kuwa Taasisi za Elimu ya Juu zinapaswa kuwa na jitihada mahususi za kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike hasa katika fani za STUH. Ili kufanikisha hili, Taasisi za Elimu ya Juu kwa kushirikiana na wadau, zinapaswa kuandaa na kutekeleza mikakati ifuatayo:

i. Kuandaa sera, kanuni na miongozo mbalimbali inayoelekeza udahili wa wanafunzi kwa kuzingatia haki usawa na uwiano wa kijinsia;

ii. Kufanya tafiti mbalimbali ili kuboresha mifumo na mikakati wezeshi inayozingatia haki usawa na uwiano wa kijinsia;

iii. Kuelimisha wadau kuhusu umuhimu wa kuzingatia haki na usawa wa kijinsia katika udahili na ubakishwaji wa wanafunzi;

iv. Kujenga uelewa na ujasiri kwa wanafunzi wa kike katika ngazi za elimu za awali kabla ya udahili kuhusu kusoma fani za STUH;

v. Kuongeza udahili na ubakishwaji wa wanafunzi unaozingatia usawa na uwiano wa kijinsia kwa kushughulikia changamoto za kiuchumi, kitaaluma, kijamii na kiafya zinazopelekea wanafunzi kushindwa kuendelea na masomo; na

vi. Kuandaa programu maalumu ya kuwapatia mafunzo ya ziada wanafunzi wa kike waliopungukiwa alama kidogo ili kukidhi vigezo vya udahili katika fani za STUH.

## 4.4 Kuzingatia Haki na Usawa wa Kijinsia katika Ajira, Kujiendeleza Kitaaluma, Kitaalamu pamoja na Majukumu ya Ufundishaji, Utafiti na Ushauri Elekezi

Katika suala la ajira na kujiendeleza kitaaluma, kitaalamu, ufundishaji, utafiti na ushauri elekezi, kumekuwa na hali ya kutokuzingatia usawa wa kijinsia. Hali hii inasababisha kutokuwepo kwa uwiano kati ya wanafunzi na watumishi wanawake na wanaume katika kupata fursa za ajira na kujiendeleza kitaaluma na kitaalamu. Aidha, kuna uwiano mdogo wa kijinsia kati ya wahadhiri wa kike na kiume katika kufanya utafiti, ushauri elekezi na kuandaa machapisho. Kwa mantiki hiyo, kuna umuhimu wa kuimarisha haki na usawa wa kijinsia ili kujenga mazingira wezeshi kwa wafanyakazi wote kushiriki kikamilifu katika ufundishaji, utafiti, ushauri elekezi, huduma kwa jamii na kutoa machapisho. Ili kufanikisha hayo, Taasisi za Elimu ya Juu kwa kushirikiana na wadau zinapaswa kufanya yafuatayo:

i. Kuandaa au kuboresha sera, kanuni, programu na miongozo mbalimbali inayotoa haki na fursa sawa katika ajira, kujiendeleza kitaaluma, kitaalamu, kufanya utafiti, ushauri elekezi na kutoa machapisho;

ii. Kuwajengea wanafunzi na wafanyakazi uwezo wa kuelewa na kutumia sera, sheria, kanuni, programu na miongozo mbalimbali inayotoa haki na fursa sawa katika ajira, kujiendeleza kitaaluma na kitaalamu;

iii. Kuandaa mazingira wezeshi kwa watumishi wanawake waliopo katika majukumu maalumu ya kijinsi kupata na kutumia fursa mbalimbali za mafunzo ya kujiendeleza na kuongeza ujuzi;

iv. Kujenga mazingira bora ya kufanyia kazi kwa watumishi wanawake wenye mahitaji maalumu ya kijinsia kama vile vyumba vya kunyonyeshea na kulishia watoto;

v. Kuwajengea uwezo watumishi wanawake kutambua na kutumia fursa za masomo ya kujiendeleza na kuongeza ujuzi;

vi. Kuandaa na kuboresha sera zinazoelekeza uwiano wa kijinsia kwenye majukumu ya utafiti, ushauri elekezi na huduma kwa jamii; na

vii. Kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wanawake kwenye majukumu ya tafiti, ushauri elekezi, huduma kwa jamii na kutoa machapisho.

## 4.5 Kuimarisha Haki, Usawa na uwiano wa Kijinsia katika Uongozi na Ushiriki katika Ngazi za Maamuzi

Uzoefu unaonesha uwepo wa changamoto na vikwazo mbalimbali vinavyosababisha ukosefu wa uwiano na usawa wa kijinsia katika nafasi za uongozi kwenye ngazi tofauti za Taasisi za Elimu ya Juu. Miongoni mwa vikwazo hivyo ni mila na desturi zenye kuleta madhara, mfumo dume, mitazamo hasi, sheria kandamizi, rushwa, dharau, pamoja na ukatili na vitendo vya udhalilishaji. Pia, kuna vikwazo vingi vinavyotokana na majukumu ya kifamilia na kijamii vinavyosababisha ukosefu wa uwiano na usawa wa kijinsia katika kushiriki kwenye uongozi na ngazi za maamuzi. Ili kukuza usawa na uwiano wa kijinsia na mazingira wezeshi, Taasisi za Elimu ya Juu kwa kushirikiana na wadau zinapaswa kufanya yafuatayo:

i. Kuanzisha au kuimarisha programu wezeshi (mentorship programme) zitakazotoa ushauri, usaidizi na usimamizi wa karibu kwa wafanyakazi wanawake ili wapate uzoefu katika uongozi na kushiriki katika kutoa maamuzi;

ii. Kuweka mifumo wezeshi ya kisera na kikanuni inayozingatia usawa na uwiano wa kijinsia katika nafasi za uongozi na ngazi mbalimbali za maamuzi; na

iii. Kuwajengea uwezo watumishi na wanafunzi wa kike kwa kuwapatia mafunzo na kozi mbalimbali za uongozi.

## 4.6 Kuimarisha Haki, Usawa na Uwiano wa Kijinsia katika Michezo na Burudani, Upatikanaji wa Elimu na Huduma za Afya ya Uzazi, Afya ya Akili, Magonjwa Yanayoambukiza na Yasiyoambukiza

Hali ya kiuchumi, ukosefu wa uwiano wa kushiriki michezo na burudani, ukosefu wa stadi za maisha, mabadiliko ya tabia nchi na mitindo ya maisha imesababisha kuongezeka kwa changamoto za afya ya uzazi, afya ya akili pamoja na magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza. Vijana wa kike na kiume wakiwemo wenye ulemavu ni miongoni mwa makundi yanaoathirika. Juhudi za makusudi zinahitajika katika kukabiliana na changamoto hizo. Ili kufikia lengo hili, Taasisi za Elimu ya Juu kwa kushirikiana na wadau zinapaswa kufanya yafuatayo:

i. Kutoa elimu inayozingatia haki,usawa na uwiano wa kijinsia juu ya stadi za maisha, afya ya uzazi, afya ya akili, magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza;

ii. Kutoa elimu inayozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia juu ya namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na athari zake;

iii. Kuhamasisha wanafunzi na wafanyakazi kufahamu hali za afya zao kwa kupima kwa hiari mara kwa mara;

iv. Kuanzisha na kuboresha huduma za stadi za maisha, afya ya uzazi, afya ya akili, magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia;

v. Kutenga maeneo, kuandaa au kuboresha miundombinu ya michezo na burudani ili kuwezesha wanaume, wanawake na watu wenye ulemavu kushiriki; na

vi. Kuanzisha, kuboresha na kuhamasisha kushiriki katika michezo na burudani za aina mbalimbali kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia.

## 4.7 Kuzingatia Usawa wa Kijinsia katika Maadili na Malezi yanayozingatia Mila na Desturi Chanya za Kitanzania

Mmomonyoko wa maadili katika Taasisi za Elimu ya Juu ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazozikabili taasisi hizo. Kwa mfano, matumizi ya madawa ya kulevya, ulevi uliopindukia pamoja na ubakaji yamekuwa ni matatizo sugu linaloendelea kushamiri miongoni mwa vijana wa kike na wa kiume kwenye Taasisi za Elimu ya Juu. Uzoefu unaoneshakuwa kumekuwa na matukio ya mauaji na kudhuru mwili kutokana na sababu za kimapenzi, ulevi na mmomonyoko wa maadili. Ili kuimarisha malezi na maadili miongoni mwa vijana katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia, Taasisi za Elimu ya Juu kwa kushirikiana na wadau zinapaswa kufanya yafuatayo:

i. Kupiga vita matumizi ya madawa ya kulevya na mapenzi ya jinsi moja;

ii. Kuweka mifumo ya kuwabaini na kuwachukulia hatua stahiki watumiaji wa madawa ya kulevya na wanaojihusisha na mahusiano ya kimapenzi ya jinsi moja;

iii. Kutoa elimu na semina za mara kwa mara juu ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevya na ulevi uliokithiri;

iv. Kuweka mifumo inayopiga vita mapenzi na mahusiano ya jinsi moja;

v. Kuanzisha na kuboresha vitengo vya ushauri na unasihi;

vi. Kuandaa mafunzo endelevu ya maadili na miiko ya kazi kwa waajiriwa wapya;

vii. Kuimarisha malezi na maadili kwa wanafunzi, wafanyakazi na watoa huduma;

viii. Kuanzisha makundi rika ya aina mabalimbali yanayokemea mmomonyoko wa maadili miongoni mwa vijana wa kike na wa kiume;

ix. Kuandaa au kuboresha kanuni za maadili katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa wanafunzi, wafanyakazi na watoa huduma;

x. Kushirikisha taasisi za kidini katika kuimarisha maadili yanayozingatia mila na desturi chanya za kitanzania; na

xi. Kuandaa na kuboresha kanzidata inayoonesha ufadhili wa masomo kwa kila mwanafunzi ili kubaini ufadhili wenye masharti yanayokiuka maadili ya Kitanzania.

## 4.8 Kuandaa na Kuboresha Mitaala na Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia kwa Kuzingatia Haki na Usawa wa Kijinsia

Wafanyakazi na wanafunzi katika Taasisi za Elimu ya Juu wanahitaji mazingira yenye miundombinu rafiki ya kufundishia, kujifunzia na kufanyia kazi yanayozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia. Baadhi ya Taasisi za Elimu ya Juu zina miundombinu isiyo rafiki hasa katika huduma za maktaba, malazi, ofisi na madarasa. Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 katika lengo namba 4 na lengo namba 5 yanaelekeza nchi kuhakikisha mifumo ya elimu yenye kuzingatia haki na usawa wa kijinsia. Pia, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023 imelenga kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia. Ili kuhakikisha uboreshaji wa miundombinu, mitaala na mbinu za ufundishaji zinazingatia haki na uwiano wa kijinsia, Taasisi za Elimu ya Juu kwa kushirikiana na wadau zinapaswa kuzingatia yafuatayo:

i. Kufanya mapitio na kuimarisha miundombinu, mitaala na mbinu za kufundishia kwa kuzingatia haki na uwiano wa kijinsia;

ii. Kuweka na kuboresha njia, mbinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia;

iii. Kuweka au kuboresha miundombinu ya kufundishia, kujifunzia na kufanyia kazi na kutolea huduma; na

iv. Kuweka au kuboresha sera, kanuni, na miongozo mbalimbali kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia.

## 4.9 Kuanzisha na Kuimarisha Huduma za Ushauri na Unasihi Zinazozingatia Haki, Usawa na Uwiano wa Kijinsia

Wahanga na waathirika wa ukatili wa kijinsia wanahitaji huduma endelevu ya ushauri na unasihi ili kuweza kukabiliana na madhara ya kimwili, kisaikolojia, kijamii na kiakili. Hata hivyo, uzoefu unaonesha kuwa huduma za ushauri na unasihi zimekuwa zikitolewa kwa kiwango kisichoridhisha. Aidha, baadhi ya taasisi zinaupungufu wa wataalamu wa huduma hizo. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Taasisi za Elimu ya Juu kwa kushirikiana na wadau zinapaswa kuchukua hatua zifuatazo:

i. Kuajiri wataalamu wa kutosha na wenye sifa stahiki za kutoa huduma za ushauri nasaha na unasihi;

ii. Kuandaa au kufanya mapitio ya Sera na Miongozo mbalimbali ya ushauri na unasihi;

iii. Kuanzisha na kuimarisha vitengo vya kutolea huduma za ushauri na unasihi kwa wanafunzi na wafanyakazi; na

iv. Kuelimisha wanajamii wa taasisi husika umuhimu wa kupata huduma za ushauri na unasihi.

## 4.10 Kuimarisha Ulinzi na Usalama kwa Kupinga na Kutokomeza Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia kwa Kuzingatia Haki na Usawa

Katika kukabiliana na matukio ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu, ni muhimu kuimarisha ulinzi na usalama unaozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia. Uzoefu unaonesha kwamba matukio ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia na vihatarishi vyake havishughulikiwi ipasavyo. Udhaifu wa mifumo ya ulinzi na usalama katika kukabiliana na changamoto za ukatili wa kijinsia umekuwa kikwazo katika kufikia malengo yanayokusudiwa. Ili kukabiliana na changamoto hizi, Taasisi za Elimu ya Juu kwa kushirikiana na wadau wanapaswa kufanya yafuatayo:

i. Kujenga uelewa wa ulinzi na usalama unaozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia;

ii. Kuandaa au kuboresha sera, sheria ndogo, kanuni, mikakati na miongozo ya ulinzi na usalama yenye kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia;

iii. Kutekeleza sera, sheria ndogo, kanuni, mikakati na miongozo ya ulinzi na usalama kwa kupinga na kupambana na ukatili na unyanyasaji wa kijinsia;

iv. Kuimarisha mifumo ya mawasiliano na utoaji wa taarifa kuhusu unyanyasaji, dhuluma, ubaguzi na uonevu unaotokana na tofauti za kijinsia;

v. Kuanzisha au kuboresha dawati la jinsia na klabu za makundi rika za kuelimisha na kupinga rushwa ya ngono; na

vi. Kuimarisha na kuhamasisha matumizi sahihi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuzuia ukatili na unyanyasaji wa kijinsia.

# SURA YA 5 UFUATILIAJI NA TATHMINI

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa msingi wa namna afua mbalimbali zitakavyotekelezwa katika Mkakati wa Usawa wa Kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Kimsingi, ufuatiliaji na tathmini unalenga kuweka mwelekeo wa utekelezaji wa afua zilizokusudiwa kwa kila eneo kwa kuzingatia Mkakati wa Usawa wa Kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu.

Ufuatiliaji na tathmini ni zoezi endelevu linalohusisha ukusanyaji wa taarifa wa shughuli za kila siku wakati wa utekelezaji wa mkakati. Zoezi hili ni muhimu ilikuonesha mwenendo wa utekelezaji na kufanya maboresho pale inaponekana kuna upungufu badala ya kusubiri tathmini ya mwisho. Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini yanapaswa kutolewa kwa wadau wote ili kuwa na uelewa wa pamoja wa utekelezaji wa mkakati huu. Vilevile, matokeo hayo yatasaidia kubaini iwapo wadau wote wanaoshiriki katika utekelezaji wa mkakati huu wanapata matokeo yaliyokusudiwa. Wizara yenye dhamana ya utekelezaji wa kutoa elimu, sayansi na teknolojia kwa kushirikiana na wadau wengine watafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Usawa wa Kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu.

## 5.2 Ufuatiliaji

Ufuatiliaji utafanyika katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mkakati huu ili kuhakikisha kuwa afua zote zilizobainishwa zinatekelezwa kama zilivyopangwa. Ufuatiliaji utafanyika kwenye matumizi ya rasilimali kwa kulinganisha na kazi zilizofanyika kwa lengo la kutathmini utekelezaji, kubainisha na kurekebisha upungufu wa kiutendaji uliojitokeza na kutoa mrejesho kwa watekelezaji. Vilevile, tathmini hufanyika kupima matokeo ya kazi zilizokamilika au zinazoendelea kulingana na vigezo vilivyowekwa. Ufuatiliaji wa mkakati utazingatia vipengele vifuatavyo:

i. Kuongeza uelewa wa dhana za masuala ya afua za kijinsia;

ii. Kuandaa na kuboresha sera, kanuni, programu, miongozo pamoja na kutenga rasilimali za utekelezaji;

iii. Kuongeza udahili na ubakishwaji wa wanafunzi unaozingatia haki na usawa wa kijinsia;

iv. Kuzingatia haki na usawa wa kijinsia katika ajira, kujiendeleza kitaaluma na kitalaamu pamoja na majukumu ya ufundishaji, tafiti na ushauri elekezi;

v. Kukuza haki na usawa wa kijinsia katika uongozi na ushiriki katika ngazi za maamuzi;

vi. Kuimarisha haki, usawa na uwiano wa kijinsia katika michezo na burudani, upatikanaji wa elimu na huduma za afya ya uzazi, afya ya akili, magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza;

vii. Kuzingatia usawa wa kijinsia katika maadili na malezi yanayozingatia mila na desturi za watanzania;

viii. Kuandaa na kuboresha mitaala, mbinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia;

ix. Kuweka na kuboresha miundombinu ya kufanyia kazi na kujifunzia inayozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia;

x. Kuanzisha na kuimarisha huduma za ushauri na unasihi zinazozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia; na

xi. Kuimarisha ulinzi na usalama kwa kupinga na kutokomeza ukatili na unyanyasaji wakijinsia kwa kuzingatia haki na usawa.

## 5.3 Tathmini

Utekelezaji wa Mkakati wa Usawa wa Kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu utafanyiwa tathmini kila baada ya miaka mitatu ili kupima uingizwaji wa masuala ya kijinsia na matokeo ya ushughulikiwaji wa vitendo vya ukatili wa Kijinsia na uzingatiaji wa haki, usawa na uwiano wa Kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu.

Aidha, tathmini itatumia viashiria vilivyowekwa katika mpango kazi kupitia malengo na shughuli zitakazoainishwa kwa ajili ya utekelezaji. Tathmini itafanyika kwa kuhusisha na kushirikiana na wadau kwa kila hatua na italenga kupima mchakato wa utekelezaji ilikuona matokeo na ufanisi na kuweza kubaini kama shabaha na malengo tarajiwa yamefikiwa, hivyo kuwezesha wasimamizi na watekelezaji kufanya maamuzi sahihi. Taarifa ya tathmini itatoa mrejesho kwa watoa maamuzi, watekelezaji na wanufaika.

Mapitio ya mkakati huu yatafanyika kila baada ya miaka mitatu au pale itakapoonekana kuna uhitaji au ulazima wa kufanya hivyo. Aidha, taasisi zitatakiwa kujifanyia tathmini kila baada ya mwaka mmoja ili kuona mafanikio na maeneo yanayohitaji kuongeza nguvu.

## 5.4 Muundo na Majukumu ya Kitaasisi

Katika utekelezaji wa mkakati huu, wizara na taasisi husika zinapaswa kuwa na majukumu yafuatayo:

### 5.4.1 Majukumu ya Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Elimu ya Juu

i. Kuandaa Mwongozo wa utekelezaji wa Mkakati huu;

ii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati huu;

iii. Kuratibu upatikanaji wa rasilimali watu na rasilimali fedha; na

iv. Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa kushirikiana na wizara yenye dhamana ya masuala ya jinsia.

### 5.4.2 Majukumu ya Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Jinsia

i. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati huu; na

ii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa kushirikiana na wizara yenye dhamana ya masuala ya elimu ya juu.

### 5.4.3 Majukumu ya Wizara zenye Taasisi za Elimu ya Juu

i. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati huu katika taasisi zilizo chini yake; na

ii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa kushirikiana na wizara yenye dhamana ya masuala ya elimu ya juu.

### 5.4.4 Majukumu ya Taasisi za Elimu ya Juu

i. Kutenga rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mkakati huu; na

ii. Kutekeleza mkakati kwa kuandaa mwongozo na mpango kazi wa utekelezaji wa mkakati huu.

### 5.4.5 Majukumu ya Wadau

i. Kuwezesha upatikanaji rasilimali fedha na utaalamu; na

ii. Kushirikiana na Taasisi za Elimu ya Juu ili ziweze kutoa elimu ya haki, usawa na uwiano wa kijinsia na kwa kuzingatia maslahi ya nchi na utamaduni wa kitanzania.

## 5.5 Utoaji wa Taarifa

Taarifa ya utekelezaji wa mkakati wa Usawa wa Kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu itatolewa kuanzia ngazi ya taasisi husika kwenda kwenye wizara yenye dhamana na

masuala ya elimu, sayansi na teknolojia. Pia, kutoa taarifa au nakala kwa wizara yenye dhamana na masuala ya maendeleo ya jamii, jinsia, wanawake na makundi maalumu kwa kila robo mwaka. Katika kuimarisha na kuongeza ufanisi wa utoaji wa taarifa ni muhimu kuzingatia matumizi ya mifumo ya kidigitali ya ukusanyaji, upokeaji, utoaji na utunzaji wa taarifa.

## 5.6 Hitimisho

Mkakati huu ni nyenzo muhimu ya kufikia haki na usawa wa kijinsia, mazingira salama na huru ya kufundishia, kujifunzia na kufanya kazi yasiyokuwa na ukatili wa kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu. Aidha, Mkakati umeainisha muundo wa utekelezaji na majukumu yake ili kuweza kuimarisha ushughulikiaji wa masuala ya usawa wa kijinsia na elimu jumuishi. Wizara yenye dhamana ya masuala ya elimu ya juu, wizara yenye dhamana ya masuala ya jinsia na wadau wengine watapaswa kushirikiana katika utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mkakati huu. Utekelezaji wa mkakati huu utawezesha kuondoa changamoto za viashiria vya kutokuwepo kwa haki, usawa na uwiano wa kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu.

# KIAMBATISHO 1: MPANGO WA UTEKELEZAJI

JEDWALI LA MPANGO WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA USAWA WA KIJINSIA KWA TAASISI ZA ELIMU YA JUU

| NA. | LENGO | MKAKATI | SHABAHA | VIASHIRIA | RASILI MALI FEDHA (Milioni) TZS | MUDA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4.1 | Kuongeza Uelewa wa Dhana za Jinsia | Kutoa elimu ya dhana za jinsia kwa kuzingatia mila na desturi chanya za kitanzania. | Elimu ya dhana za jinsia kwa kuzingatia mila na desturi chanya iwe imetolewa ifikapo Juni, 2029. | - Idadi ya taarifa za mafunzo ya dhanazajinsia | 250 | Juni, 2029. | WEST, WMJJWM na Taasisi za Elimu ya Juu |
| | | | | Idadi ya wafanyakazi, wanafunzi na wanajumuia wengine waliofikiwa na mafunzo ya dhana za jinsia | | | |
| | | Kuingiza masuala ya kijinsia katika shughuli zote za taasisi. | Masuala ya kijinsia yawe yameingizwa katika shughuli zote za taasisi ifikapo Juni, 2029. | Idadi ya shughuli zilizotekelezwa kwa kuzingatia masuala ya kijinsia. | | | |
| | | Kuwajengea uwezo wanajumuiya wa taasisi kuhusu utambuzi na huduma stahiki kwa watu wenye mahitaji maalumu. | Wanajumuiya wa taasisi wamejengewa uwezo kuhusu utambuzi na utoaji huduma stahiki kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia ifikapo Juni, 2029. | Idadi ya wanajumuiya wa taasisi waliojengewa uwezo. | | | |
| 4.2 | Kuandaa na kuboresha sera, kanuni, mipango, programu, miongozo pamoja na kutenga rasilimali za utekelezaji | Kuandaa na kuboresha sera, kanuni, mipango, programu, na miongozo inayozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia. | Sera, kanuni, mipango, programu na miongozo imeandaliwa na kuboreshwa kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya sera, Kanuni, mipango, programu na miongozo iliyoandaliwa na kuboreshwa kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia. | 150 | Juni, 2030. | WEST, WMJJWM na Taasisi za Elimu ya Juu |
| | | Kujenga uelewa kwa wanajumuiya kuhusu uwepo, umuhimu na matumizi ya nyaraka hizo. | Uelewa kuhusu uwepo, umuhimu na matumizi ya nyaraka zinazozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia uwe umejengeka ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya watu wanaotumia nyaraka zenye kuzingatia masuala ya jinsia. | | | |

| NA. | LENGO | MKAKATI | SHABAHA | VIASHIRIA | RASILI MALI FEDHA (Milioni) TZS | MUDA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa kuandaa na kuboresha nyaraka hizo. | Kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili ya utekelezaji ifikapo Juni, 2030. | Kiasi cha rasilimali kilichotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mkakati. | | | |
| 4.3 | Kuongeza Udahili na Ubakishwaji wa Wanafunzi Unaozingatia Haki, Uwiano na Usawa wa Kijinsia | Kuandaa sera, kanuni na miongozo mbalimbali inayoelekeza udahili wa wanafunzi kwa kuzingatia haki usawa na uwiano wa kijinsia. | Sera, kanuni na miongozo inayoelekeza udahili wa wanafunzi kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia ziwe zimeandaliwa ifikapo Juni, 2029. | Idadi ya sera, kanuni na miongozo inayoelekeza udahili wa wanafunzi kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia. | 330 | Juni, 2029. | WEST, WMJJWM na Taasisi za Elimu ya Juu |
| | | Kufanya tafiti mbalimbali ili kuboresha mifumo na mikakati wezeshi inayozingatia haki usawa na uwiano wa kijinsia. | Tafiti mbalimbali zimefanyika ili kuboresha mifumo na mikakati wezeshi inayozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia ziwe zimefanyika ifikapo Juni, 2029. | Idadi ya tafiti zenye lengo la kuboresha mifumo na mikakati wezeshi inayozingatia haki, usawa na uwiano wa Kijinsia. | | | |
| | | Kuelimisha wadau kuhusu umuhimu wa kuzingatia haki na usawa wa kijinsia katika udahili na ubakishwaji wa wanafunzi. | Wadau wawe wamepata elimu kuhusu umuhimu wa kuzingatia haki na usawa wa kijinsia katika udahili na ubakishwaji wa wanafunzi ifikapo Juni, 2029. | Idadi ya wadau walioelimishwa kuhusu umuhimu wa kuzingatia haki na usawa wa kijinsia katika udahili na ubakishwaji wa wanafunzi. | | | |
| | | Kujenga uelewa na ujasiri kwa wanafunzi wa kike katika ngazi ya elimu msingi kuhusu kusoma fani za STUH. | Kujenga uelewa na ujasiri kwa wanafunzi wa kike katika ngazi ya elimu msingi kuhusu kusoma fani za STUH ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya wanafunzi wa kike kwenye ngazi ya elimu msingi waliojengewa uwezo kuhusu umuhimu wa kusoma fani za STUH | | | |

| NA. | LENGO | MKAKATI | SHABAHA | VIASHIRIA | RASILI MALI FEDHA (Milioni) TZS | MUDA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kuongeza udahili na ubakishwaji wa wanafunzi unaozingatia usawa na uwiano wa kijinsia kwa kushughulikia changamoto za kiuchumi, kitaaluma, kijamiina kiafya zinazopelekea wanafunzi kushindwa kuendelea na masomo. | Programu maalumu ya kuwapatia mafunzo ya ziada wanafunzi wa kike waliopungukiwa alama ili kukidhi vigezo vya udahili katika fani za STUH iwe imeandaliwa ifikapo Juni, 2030. | Programu maalumu ya mafunzo ya ziada iliyoandaliwa kwa ajili ya wanafunzi wa kike | | | |
| | | Kuandaa programu maalumu ya kuwapatia mafunzo ya ziada wanafunzi wa kike waliopungukiwa alama kidogo ili kukidhi vigezo vya udahili katika fani za STUH. | Programu ya mafunzo imeandaliwa na kutekelezwa ifikapo Juni, 2030. | Programu ilioyoandaliwa na idadi ya wanafunzi waliofikiwa na programu. | | | |
| 4.4 | Kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia katika ajira, kujiendeleza kitaaluma na kitalaamu pamoja na majukumu ya ufundishaji, tafiti na ushauri elekezi | Kuandaa au kuboresha sera, kanuni, programu na miongozo mbalimbali inayotoa haki na fursa sawa katika ajira, kujiendeleza kitaaluma na kitaalamu; kufanya utafiti, ushauri elekezi na kutoa machapisho. | Sera, kanuni na miongozo inayotoa haki na fursa sawa katika ajira na kujiendeleza kitaaluma na kitaalamu na uwezeshaji wa wanataaluma wanawake kushiriki kikamilifu katika majukumu kufanya tafiti na ushauri elekezi iwe imeanzishwa na kuboreshwa ifikapo Juni, 2030. | Sera, kanuni na miongozo iliyopitishwa na mamlaka za taasisi zenye maudhui yanayozingatia haki na fursa sawa. | 150 | Juni, 2030. | Taasisi za Elimu ya Juu |

| NA. | LENGO | MKAKATI | SHABAHA | VIASHIRIA | RASILI MALI FEDHA (Milioni) TZS | MUDA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kuwajengea wanafunzi na wafanyakazi uwezo wa kuelewa na kutumia sera, sheria, kanuni, programu na miongozo mbalimbali inayotoa haki na fursa sawa katika ajira, kujiendeleza kitaaluma na kitaalamu. | Wanafunzi na wafanyakazi wamejengewa uwezo wa kuelewa na kutumia sera, kanuni na miongozo inayotoa haki na fursa sawa katika ajira na kujiendeleza kitaaluma na kitaalamu ifikikapo Juni, 2030. | Idadi ya wanafunzi na wafanyakazi waliojengewa uwezo wa kuelewa na kutumia sera, kanuni na miongozo inayotoa haki na fursa sawa katika ajira na kujiendeleza kitaaluma na kitaalamu. | | | |
| | | Kuandaa mazingira wezeshi kwa wanawake waliopo katika majukumu maalumu ya kijinsi kupata na kutumia fursa mbalimbali za mafunzo ya kujiendeleza na kuongeza ujuzi. | Kutafuta na kutengeneza fursa za mafunzo ya kujiendeleza na kuongeza ujuzi ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya wanawake waliopata na kuzitumia fursa za mafunzo ya kujiendeleza na kuongeza ujuzi. | | | |
| | | Kuwajengea wafanyakazi wa kike uwezo wa kutambua na kutumia fursa za masomo ya kujiendeleza na kuongeza ujuzi | Elimu ya kijinsia kuhusu haki, kanuni, mifumo na fursa za ajira imetolewa ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya programu maalumu za kuwawezesha wanataaluma wanawake kuandaa machapisho. | | | |
| | | Kujenga mazingira bora yakufanyia kazi kwa wanawake wenye mahitaji maalumu ya kijinsia kama vile vyumba vya kunyonyeshea na kulishia watoto. | Kuandaa maeneo kwa ajili ya wanawake wenye mahitaji maalumu ya kijinsia kama vile vyumba vya kunyonyeshea na kulishia watoto ifikapo Juni, 2030. | Maeneo yaliyoandaliwa kwa ajili ya wanawake wenye mahitaji maalumu ya kijinsia kama vile vyumba vya kunyonyeshea na kulishia watoto. | | | |

| NA. | LENGO | MKAKATI | SHABAHA | VIASHIRIA | RASILI MALI FEDHA (Milioni) TZS | MUDA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kuandaa na kuboresha sera zinazoelekeza uwiano wa kijinsia kwenye majukumu ya utafiti, ushauri elekezi na huduma kwa jamii. | Kuwa na sera na miongozo inayoonesha uwiano wa majukumu na ushiriki wenye uwiano kwenye kufanya tafiti, kutoa ushauri elekezi na huduma za jamii ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya sera kanuni na miongozo itakayotolewa kuwawezesha wanawake wanataaluma kufanya utafiti na ushauri elekezi. | | | |
| | | Kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wanawake kwenye majukumu ya utafiti, ushauri elekezi, huduma kwa jamii na kutoa machapisho. | Kuwa na programu ya mafunzo ya kujenga uwezo ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya wafanyakazi wanawake waliojengewa uwezo | | | |
| 4.5 | Kuimarisha haki, usawa na uwiano wa Kijinsia katika Uongozi na Ushiriki katika Ngazi za Maamuzi | Kuanzisha au kuimarisha" programu za ushauri wezeshi (*mentorship programme)* kwa kuwapa usaidizi na usimamizi wa karibu kwa wafanyakazi wanawake ili wapate uzoefu katika uongozi na kushiriki katika kutoa maamuzi. | Kuwa na programu zilizopitishwa na menejementi kwa ajili ya ushauri wezeshi zenye kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya programu iliyoandaliwa | 210 | Juni, 2030. | WEST, Taasisi za Elimu ya Juu |
| | | Kuweka mifumo wezeshi ya kisera na kikanuni inayozingatia usawa na uwiano wa kijinsia katika nafasi za uongozi na ngazi mbalimbali za maamuzi. | Kuwa na sera na kanuni zinazosimamia upatikanaji wa viongozi na watoa mamauzi zenye kuzingatia haki, usawa na uwiano wa Kijinsia ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya sera na kanuni au vipengele kwenye sera na kanuni | | | |

| NA. | LENGO | MKAKATI | SHABAHA | VIASHIRIA | RASILI MALI FEDHA (Milioni) TZS | MUDA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kuwajengea uwezo watumishi na wanafunzi wa kike kupata mafunzo na kozi mbalimbali za uongozi. | Watumishi na wanafunzi wamepatiwa mafunzo mbalimbali yenye kuwajengea uwezo wa uongozi ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya watumishi na wanafunzi walioshiriki katika mafunzo | | | |
| 4.6 | Kuimarisha haki, usawa na uwiano wa kijinsia katika michezo na burudani, upatikanaji wa elimu na huduma za afya ya uzazi, afya ya akili, magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza | Kutoa elimu inayozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia juu ya stadi za maisha, afya ya uzazi, afya ya akili, magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza. | Kutoa elimu juu ya stadi za maisha, afya ya uzazi, afya ya akili, magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza imetolewa ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya wanajumuiya katika Taasisi ya Elimu ya Juu waliopata elimu na kutumia huduma za, afya ya uzazi, afya ya akili, magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza. | 70 | | Taasisi za Elimu ya Juu |
| | | Kutoa elimu inayozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia juu ya namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na athari zake. | Kuandaa na kutekeleza programu ya elimu inayozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia juu ya namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na athari zake ifikapo Juni, 2030. | Programu iliyoandaliwa na kuidhinishwa na mamlaka za Taasisi. | | | |
| | | | | Idadi ya washiriki waliopatiwa mafunzo | | | |
| | | Kuhamasisha wanafunzi na wafanyakazi kufahamu hali za afya zao kwa kupima kwa hiari mara kwa mara. | Wanafunzi na wafanyakazi wamehamasika kufahamu hali za afya zao kwa kupima kwa hiari mara kwa mara ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya wanafunzi na wafanyakazi waliopima na kutambua hali za afya zao. | | | |

| NA. | LENGO | MKAKATI | SHABAHA | VIASHIRIA | RASILI MALI FEDHA (Milioni) TZS | MUDA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kuanzisha na kuboresha huduma za stadi za maisha, afya ya uzazi, afya ya akili, magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia. | Huduma za stadi za maisha, afya ya uzazi, afya ya akili, magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza zimeanzishwa na kuboreshwa ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya huduma za stadi za maisha, afya ya uzazi, afya ya akili, magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza zilizoanzishwa na kuboreshwa | | | |
| | | Kutenga maeneo, kuandaa au kuboresha miundombinu ya michezo na burudani ili kuwezesha wanaume, wanawake na watu wenye ulemavu kushiriki. | Maeneo yametengwa na miundombinu ya michezo na burudani yenye kuzingatia haki, usawa na uwiano wa Kijinsia imewekwa ifikapo Juni, 2030. | Ukubwa wa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya michezo. | | | |
| | | | | Idadi ya miundombinu ya michezo inayowezesha haki, usawa na uwiano wa kijinsia. | | | |
| | | Kuanzisha, kuboresha na kuhamasisha kushiriki katika michezo na burudani za aina mbalimbali kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia. | Michezo na burudani za aina mbalimbali zimeanzishwa, kuboreshwa na kuhamasishwa ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya michezo na burudani zilizoanzishwa na kuboreshwa. | | | |

| NA. | LENGO | MKAKATI | SHABAHA | VIASHIRIA | RASILI MALI FEDHA (Milioni) TZS | MUDA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4.7 | Kuzingatia usawa wa kijinsia katika maadili na malezi yanayo zingatia mila na desturi chanya za kitanzania. | Kupiga vita matumizi ya madawa ya kulevya na mapenzi ya jinsi moja. | Vita dhidi ya madawa ya kulevya na mahusiano ya kimapenzi yanayokinzana na mila na desturi za kitanzania imefanikiwa ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya mifumo iliyowekwa ya kuwabaini watumiaji wa madawa ya kulevya na wanaojihusisha na mahusiano ya kimapenzi yanayokinzana na mila na desturi za kitanzania. | 220 | Juni, 2030. | WEST, WMJJWM na Taasisi za Elimu ya Juu |
| | | Kuweka mifumo ya kuwabaini na kuwachukulia hatua stahiki watumiaji wa madawa ya kulevya na wanaojihusisha na mahusiano ya kimapenzi ya jinsi moja. | Mifumo ya kuwabaini na kuwachukulia hatua stahiki watumiaji wa madawa ya kulevya na wanaojihusisha na mahusiano ya kimapenzi yanayokinzana na mila na desturi za kitanzania imewekwa ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya kampeni zilizofanikiwa za kupiga vita madawa ya kulevya na mahusiano ya kimapenzi yanayokinzana na mila na desturi za kitanzania. | | | |
| | | Kutoa elimu na semina za mara kwa mara juu ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevya na ulevi uliokithiri. | Elimu na semina za mara kwa mara juu ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevya na ulevi uliokithiri ifikapo Juni, 2030. | Taarifa za elimu na semina zilizotolewa katika Taasisi za Elimu ya Juu. | | | |
| | | Kuweka mifumo inayopiga vita mapenzi na mahusiano ya jinsi moja. | Mifumo inayopiga vita mapenzi na mahusiano ya jinsi moja hadi ifikapo Juni, 2030. | Uwepo mifumo inayopiga vita mapenzi na mahusiano ya jinsi moja. | | | |
| | | Kuanzisha na kuboresha vitengo vya ushauri na unasihi. | Vitengo vya ushauri na unasihi viwepo hadi ifikapo Juni, 2028. | Uwepo wa vitengo vya ushauri na unasihi. | | | |

| NA. | LENGO | MKAKATI | SHABAHA | VIASHIRIA | RASILI MALI FEDHA (Milioni) TZS | MUDA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kuandaa mafunzo endelevu ya maadili na miiko ya kazi kwa waajiriwa wapya. | Mafunzo endelevu ya maadili na miiko ya kazi kwa waajiriwa wapya yafanyike kila mwaka. | Taarifa za mafunzo endelevu ya maadili na miiko ya kazi kwa waajiriwa wapya. | | | |
| | | Kuimarisha malezi na maadili kwa wanafunzi, wafanyakazi na watoa huduma. | Mbinu za kuimarisha malezi na maadili kwa wanafunzi, wafanyakazi na watoa huduma. | Taarifa za uimarishwaji malezi na maadili kwa wanafunzi, wafanyakazi na watoa huduma. | | | |
| | | Kuanzisha makundi rika ya aina mabalimbali yanayokemea mmomonyoko wa maadili miongoni mwa vijana wa kike na wa kiume. | Makundi rika ya aina mabalimbali yanayokemea mmomonyoko wa maadili miongoni mwa vijana wa kike na wa kiume. | Uwepo wa makundi rika ya aina mabalimbali yanayokemea mmomonyoko wa maadili miongoni mwa vijana wa kike na wa kiume. | | | |
| | | Kuandaa au kuboresha kanuni za maadili katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa wanafunzi, wafanyakazi na watoa huduma. | Kuboresha kanuni za maadili katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa wanafunzi, wafanyakazi na watoa huduma. | Taarifa za kuboreshwa au kuandaliwa kwa kanuni za maadili katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa wanafunzi, wafanyakazi na watoa huduma. | | | |
| | | Kushirikisha taasisi za kidini katika kuimarisha maadili yanayozingatia mila na desturi chanya za kitanzania. | Taasisi za kidini kushiriki katika kuimarisha maadili yanayozingatia mila na desturi chanya za kitanzania. | Taarifa za ushirikishwaji wa taasisi za kidini katika kuimarisha maadili yanayozingatia mila na desturi chanya za kitanzania. | | | |
| | | Kuandaa na kuboresha kanzi data inayoonesha ufadhili wa masomo kwa kila mwanafunzi ili kubaini ufadhili wenye masharti yanayokiuka maadili ya Kitanzania. | Kanzidata inayoonesha ufadhili wa masomo kwa kila mwanafunzi inaandaliwa na kuboreshwa kila mwaka. | Uwepo wa kanzidata inayoonesha ufadhili wa masomo kwa kila mwanafunzi. | | | |

| NA. | LENGO | MKAKATI | SHABAHA | VIASHIRIA | RASILI MALI FEDHA (Milioni) TZS | MUDA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4.8 | Kuandaa na kuboresha mitaala na mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia haki na usawa wa kijinsia. | Kufanya mapitio na kuimarisha mitaala inayozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia. | Mitaala inayozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia iwe imefanyiwa mapitio na kuimarishwa ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya mitaala inayozingatia haki, usawa na uwiano wa Kijinsia | 290 | Juni, 2030. | WEST, WMJJWM na Taasisi za Elimu ya Juu |
| | | Kuweka na kuboresha njia, mbinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia | Mbinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia ziwe zimewekwa na kuboreshwa ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya vifaa na mbinu za kufundishia kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa Kijinsia | | | |
| | | Kuweka au kuboresha miundombinu ya kufundishia, kujifunzia na kufanyia kazi na kutolea huduma. | Miundombinu ya kufundishia, kujifunzia, kufanyia kazi na kutolea huduma iwe imeimarishwa na kuboreshwa ifikapo Juni, 2030. | Miundombinu ya kufundishia, kujifunzia, kufanyia kazi na kutolea huduma iliyoimarishwa na kuboreshwa na kupitishwa na mamlaka husika. | | | |
| | | Kuweka au kuboresha sera, kanuni, na miongozo mbalimbali kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia. | Sera, kanuni na miongozo inayozingatia haki, usawa na uwiano wa Kijinsia iwe imeandaliwa na kuboreshwa ifikapo Juni, 2030. | Sera, kanuni na miongozo iliyopitishwa na mamlaka husika. | | | |
| 4.9 | Kuimarisha na kuanzisha huduma za Ushauri na Unasihi zinazozingatia Haki, Usawa na uwiano wa Kijinsia | Kuajiri wataalamu wa kutosha na wenye sifa stahiki wa huduma za ushauri nasaha na unasihi. | Wataalamu wa kutosha na wenye sifa stahiki wawe wameajiriwa ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya wataalamu walioajriwa | 450 | Juni, 2030. | Taasisi za Elimu ya Juu |

| NA. | LENGO | MKAKATI | SHABAHA | VIASHIRIA | RASILI MALI FEDHA (Milioni) TZS | MUDA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kuandaa au kufanya mapitio ya sera, na miongozo mbalimbali ya ushauri na unasihi. | Sera, kanuni, na miongozo mbalimbali kwa kuzingatia haki, usawa na uwiano wa Kijinsia ziwe zimeandaliwa au kuboreshwa ifikapo Juni, 2030. | Idadi ya Sera, kanuni na miongozo inayozingatia hakina usawa na uwiano wa Kijinsia. | | | |
| | | Kuanzisha na kuimarisha vitengo vya kutolea huduma za ushauri na unasihi kwa wanafunzi na wafanyakazi. | Vitengo vya kutolea huduma za ushauri na unasihi kwa wanafunzi na wafanyakazi viwe vimeimarishwa ifikapo Juni, 2029. | Taarifa ya utekelezaji | | | |
| | | Kuelimisha wanajamii wa taasisi husika umuhimu wa kupata huduma za ushauri na unasihi. | Wanajamii wawe wamepata Elimu juu ya huduma ya ushauri na unasihi ifikapo Juni, 2029. | Idadi ya wanajamii waliopata Elimu ya huduma ya ushauri na unasihi. | | | |
| 4.10 | Kuimarisha ulinzi na usalama kwa kupinga na kutokomeza ukatili na unyanyasaji wa kijinsia kwa kuzingatia haki na usawa | Kujenga uelewa wa ulinzi na usalama unaozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia | Kuandaa au kuboresha programu ya kuwajengea uelewa wa ulinzi na usalama unaozingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia ifikapo Juni, 2030. | Programu iliyoandaliwa na idadi ya watu waliofikiwa na kujengewa uelewa kwenye Taasisi ya Elimu ya Juu. | 310 | Juni, 2030. | WEST, WMJJWM na Taasisi za Elimu ya Juu |
| | | Kuandaa au kuboresha sera, sheria ndogo, kanuni, mikakati na miongozo ya ulinzi na usalama yenye kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia | Sera, sheria ndogo, kanuni na miongozo ya ulinzi na usalama yenye kuzingatia haki, usawa na uwiano wa kijinsia iwe imeandaliwa ifikapo Juni, 2030 | Idadi ya sera na miongozo ya ushauri na unasihi iliyoanzishwa na kupitiwa na mamlaka za taasisi. | | | |

| NA. | LENGO | MKAKATI | SHABAHA | VIASHIRIA | RASILI MALI FEDHA (Milioni) TZS | MUDA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kutekeleza sera, sheria ndogo, kanuni, mikakati na miongozo ya ulinzi na usalama kwa kupinga na kupambana na ukatili na unyanyasaji wa kijinsia | Miongozo ya Serikali juu ya kupinga na kupambana na ukatili na unyanyasaji wa kijinsia iwe inatekelezwa ifikapo Juni, 2030. | Taarifa ya utekelezaji ya kila robo mwaka, nusu mwaka na mwaka. | | | |
| | | Kuimarisha mifumo ya mawasiliano na utoaji wa taarifa kuhusu unyanyasaji, dhuluma, ubaguzi na uonevu unaotokana na tofauti za kijinsia. | Kuhakikisha uwepo wa mifumo yenye kuweka mawasiliano na utoaji wa taarifa kuhusu unyanyasaji, dhuluma na ubaguzi wa kijinsia ifikapo Juni, 2029. | Taarifa ya uwepo wa mifumo. | | | |
| | | Kuanzisha au kuboresha dawati la jinsia na klabu za makundi rika za kuelimisha na kupinga rushwa ya ngono. | Uanzishwaji wa dawati la jinsia, makundi rika na klabu za kuelimisha na kupinga rushwa yawe yameanzishwa ifikapo Juni, 2028. | Idadi ya watu walioripoti kwenye dawati la Jinsia kuhusu vitendo vya Kijinsia. | | | |
| | | Kuimarisha na kuhamasisha matumizi sahihi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuzuia ukatili na unyanyasaji wa kijinsia | Mfiumo ya TEHAMA ya kushughulikia matukio ya ukatili wa Kijinsia imeanzishwa ifikapo Juni, 2030. | Taarifa ya utekelezaji na idadi ya mifumo iliyoanzishwa. | | | |

**WIZARA YA ELIMU,
SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**Mji wa Serikali
Mtumba - Mtaa wa Afya
S.L.P 10
40479 Dodoma, Tanzania**

**info@moe.go.tz
www.moe.go.tz**